

EWURA YAADHIMISHA SIKU YA WANAWAKE DUNIANI 2019

Wanawake wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) wameungana na wanawake wengine duniani kote kuenzi na kusherehekea Siku ya Wanawake Duniani inayoadhimishwa leo tarehe 8 Machi, 2019, yenye kauli mbiu “**Badili Fikra Kufikia Usawa wa Kijinsia kwa Maendeleo Endelevu**”

Wanawake wa EWURA wameadhimisha siku hii adhimu kwa kushiriki katika kikao cha wanawake kilichofanyika Makao Makuu ya Mamlaka na katika Ofisi za Kanda, kilichojadili namna ya kuongeza ufanisi katika utendaji kazi, kuimarisha ushirikiano na umoja katika kutatua changamoto mbalimbali zinazowakabili na zile zinazoikabili jamii katika sekta za Nishati na Maji.

Kwa niaba ya Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa EWURA, Mkurugenzi wa Masuala ya Umeme, Godfrey Chibulunje amewatumia salamu na pongezi wanawake wote wa EWURA kwa kuweza kuadhimisha siku hii muhimu katika ustawi wao na wanawake wote.

Chibulunje ameeleza kuwa, EWURA inaienzi siku ya wanawake kwa kuendelea kuimarisha mazingira na kuhamasisha uwekezaji katika nishati jadidifu ili kuwapunguzia wanawake adha ya kutafuta kuni na kuwafanya kuachana na matumizi ya kuni na mkaa kwa lengo la kuhifadhi na kulinda mazingira pamoja na afya zao.

Chibulunje ameeleza kuwa EWURA inatambua na kuthamini mchango wa wanawake katika jamii, ambao umekuwa ni kielelezo cha utendaji kazi wenye ufanisi wa hali ya juu na chachu kwa Mamlaka kufikia azma yake ya “ Kuwa Mdhibiti Bora wa Kiwango cha Kimataifa katika sekta za Nishati na Maji.”

“Mafanikio ya Mamlaka hayawezi kutajwa bila juhudi na jitihada za wanawake tulio nao hapa leo ambao wamekuwa mfano wa kuigwa kwa uwajibikaji na utendaji kazi wao wa hali ya juu unaoifanya EWURA kuwa miongoni mwa Mamlaka zinazofanya vizuri. Tutaendelea kutoa ushirikiano kwa wanawake wote na kuamasisha uwekezaji katika Nishati jadidifu kwa ustawi wa wanawake na jamii kwa ujumla.” Amesisitiza Chibulunje.

Aidha, Chibulunje amewataka wanawake kuendelea kuwa wabunifu zaidi na kuongeza juhudi na maarifa katika utendaji, kudumisha mshikamano na ushirikiano kwa maendeleo endelevu ya wanawake na taifa kwa ujumla.

Naye Meneja Rasilimali Watu na Utawala wa EWURA, Christina Nderumaki kwa niaba ya wanawake wote, ameishukuru Mamlaka kwa kuendelea kutoa ushirikiano kwa wanawake na kueleza kuwa, ili maendeleo endelevu ya wanawake yaweze kufikiwa ni lazima kila mwanamke awe na fikra chanya katika utekelezaji wa majukumu yake ya kila siku.

Nderumaki amewakumbusha wanawake kuwa utetezi wa haki zao unapaswa kufanywa kwa kutii miongozo na kanuni za utendaji kazi na kuwa utekelezaji wake ni sambamba na ulinzi wa haki za wengine; na hii ndio itakayoifanya jamii kuona na kutambua thamani na mchango wa wanawake.